


NOTISI KUHUSU TARATIBU ZA UCHUKUAJI, UJAZAJI NA UREJESHAJI WA FOMU ZA

MAOMBI YA NAFASI ZA JUU ZA UONGOZI WA CHAMA - TAPSEA

Kwa mujibu wa Katiba ya Chama cha Makatibu Mahsusi ya mwaka 2015 sehemu ya Nne, Kifungu cha Kumi (10), kikisomwa pamoja na Kanuni za Chama za Mwaka 2021, Sura ya Tatu (3), Kifungu cha 8- 10, Notisi namba **TAPSEA/2026/GE/N. 04** inatolewa kuhusu taratibu za **uchukuaji, ujazaji na urejeshaji** wa fomu za maombi kwa **WATANIA** kama zifuatavyo:

- i. Mwanachama anayetaka kugombea uongozi atapaswa ajaze fomu maalum ya maombi ya nafasi anayotaka kwa maelekezo yanayoambatana na nafasi husika anayoiomba.
- ii. Fomu za kugombea Uongozi zitatolewa baada ya kulipa kiasi cha Shilingi **150,000/=** kwa wanaotiania katika nafasi za juu za Uongozi wa Chama yaani: **Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mweka Hazina, pamoja na Wajumbe tisa (9) wa Baraza.**
- iii. Fomu zitatolewa na Katibu Mkuu wa Chama baada ya mtiania kuwasilisha stakabadhi ya malipo ya gharama ya fomu yaliyofanywa kwenye akaunti za Chama Namba: **TANZANIA PERSONAL SECRETARIES ASSOCIATION, CRDB BANK Plc, TAWI LA AZIKIWE, 0150031411800 AU TANZANIA PERSONAL SECRETARIES ASSOCIATION, TAWI LA NMB HOUSE, 22306600363.** Kila fomu itakuwa na **namba bainifu**, hivyo hairuhusiwi kugawa malipo au fomu kwa mgombea mwingine.
- iv. Zoezi la kuchukua, kujaza na kurejesha fomu linaanza rasmi leo **Ijumaa, tarehe 13/02/2026** na kufungwa Jumatatu, **tarehe 02/03/2026 saa kumi kamili jioni. (10.00 jioni).**
- v. Kila nafasi itagombewa peke yake, Mtiania anapaswa achukue fomu kwa nafasi moja tu na kwamba hairuhusiwi kuchukuliwa au kurejeshewa fomu na mtu mwingine.
- vi. Inashauriwa fomu zirejeshwe kwa kutumia EMS, au kwa kupokelewa na kusainisha kwenye kitabu **"dispatch"** zikiwa zimefungwa kwenye bahasha mbili kama itumwavyo barua za siri, bahasha ya juu ielekezwe kwa Katibu Mkuu -TAPSEA na bahasha ya Ndani kwa Mwenyekiti, Kamati ya Uchaguzi – TAPSEA 2026.
- vii. Fomu zitakazo chelewa kutumwa hazitapokelewa.
- viii. Mtiania azingatia mahitaji na masharti yaliyotolewa katika fomu ya maombi kwa ukamilifu. Kushindwa kuzingatia maelekezo hayo, fomu haita shughulikiwa kwa hatua zingine.
- ix. Mtiania akihitaji maelekezo ya ziada tafadhali awasiliane na Katibu Mkuu wa Chama na si vinginevyo. Vilevile, mtiania aepuke kuomba ufafanuzi kupitia Makundi ya Mtandao kwa kuwa itakuwa vigumu kutoa maelekezo kuhusu changamoto alizonazo.
- x. Anuani itakayotumika kurejesha fomu au kwa mawasiliano zaidi ni anuani ya Chama, yaani: Katibu Mkuu – TAPSEA. Nyumba ya Maarifa (NIP), Mkabala na ATCL House, Ghorofa ya kwanza, Mtaa wa Ohio. Ilala - DAR ES SALAAM. S.L.P 79868, Dar es Salaam, Tanzania. Simu: +255 22 2127464, Nukushi: +255 22 2126399; Barua pepe: tapsea2014@gmail.com: Tovuti: <http://www.tapsea.or.tz>

Karibuni tuanze mchakato wa kuimarisha Demokrasia katika Chama chetu



Charles George Magaya

MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHAGUZI - TAPSEA

13/02/2026

